JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegrams "AFYA", **DODOMA**
Nambari ya simu: **255-026-2323267/2351196**
Fax Na.255-22-2138060
(Barua zote ziandikwe kwa **Katibu Mkuu**)

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Maendeleo ya Jamii,
Jengo la 11,
S.L.P 743,
40478 DODOMA.

16 Mei 2019

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UGONJWA WA HOMA YA DENGUE HAPA NCHINI, ILIYOTOLEWA NA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Ndugu Wanahabari na Wananchi,

Leo tumekutana hapa kwa ajili ya kutoa taarifa juu ya mwenendo wa ugonjwa wa Homa ya Dengue nchini, hususani katika mikoa iliyoathirika na ugonjwa huu hasa mkoa wa Dar es Salaam na Tanga. Hivyo nichuke fursa hii kuwahabarisha wananchi hali na mwenendo wa ugonjwa huu na kuwakumbusha mambo muhimu ya kufanya katika kuudhibiti.

Ndugu wanahabari na wananchi,

Kufuatia tamko letu tulilolitoa tarehe 10 Mei 2019, tumeona ni vyema kuwapa tena taarifa ya mwenendo na hali ya ugonjwa huu, na kwa bahati nzuri tumewaalika wenzetu wa Dar es Salaam ili kufafanua baadhi ya hatua wanazochukua katika kudhibiti ugonjwa huu.

Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2019 tangu kutokea kwa ugonjwa huu mwezi Januari 2019 kati ya watu waliopimwa, jumla ya wagonjwa 1,901 wamethibishwa kuwa

na virusi au walikwishapata ugonjwa wa Dengue na kati ya hao **1,809** ni kutoka Dar Es Salaam, **89** ni kutoka Tanga **1** kutoka Singida, **1** Kilimanjaro na 1 ni Pwani Aidha wagonjwa waliopatikana katika mikoa ya Pwani na Kilimanjaro wote walitokea Dar es Salaam. Mpaka sasa hakuna vifo zaidi vilivyotokea tangu tulivyotoa taarifa wiki iliyopita.

Takwimu za ugonjwa wa Homa ya Dengue kwa kipindi cha siku 9 tangu tutoe tamko tumepata wagonjwa 674 sawa na wastani wa wagonjwa 75 kwa kila siku hii ikiwa ni tofauti na wastani wa wagonjwa 32 waliopatikana mwezi Aprili. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa uelewa kuhusu ugonjwa huu kwa wananchi walio wengi wenye dalili na hivyo wanajitokeza kupata huduma za uchunguzi ambazo zimeendelea kupanuka kwenye vituo vyetu katika mkoa wa Dar es Salaam na Tanga. Idadi ya vituo vinavyopima ugonjwa huu imeongezeka hadi kufikia **19** tofauti na vituo **7** vya awali

Ndugu Wanahabari na Wananchi,

Nipende kuwakumbusha tena kuwa Ugonjwa wa Dengue unaenezwa na mbu aina ya **Aides** mbu mweusi mwenye madoa doa meupe ya kung'aa, ambaye hupendelea kuuma hasa wakati wa asubuhi, mchana na jioni.

Dalili za ugonjwa huu ni pamoja na **homa ya ghafla, kuumwa na kichwa hususani sehemu za macho**, **maumivu ya viungo na uchovu.** Dalili hizi huanza kujitokeza kati siku ya 3 hadi 14 tangu mtu alipoambukizwa virusi vya homa ya Dengue.

Wakati mwingine dalili za ugonjwa huu zinaweza kufanana sana na dalili za ugonjwa wa **Malaria,** hivyo basi wananchi wanaaswa kuwa makini pindi wapatapo homa, **wahakikishe wanakwenda kupata huduma kwenye**

vituo vya kutolea huduma za afya, ili waweze kufanyiwa uchunguzi stahiki kupatiwa tiba sahihi.

Aidha, mara chache hutokea mgonjwa wa homa ya dengue, anapata vipele vidovidogo, anavilia damu kwenye ngozi na wengine **kutokwa na damu** sehemu za fizi, mdomoni, puani, kwenye macho na pia kwenye njia ya haja kubwa au ndogo. Katika mlipuko huu uliotokea nchini wagonjwa wengi hawana dalili za kutokwa damu au kuvilia damu kwenye ngozi

Ndugu Wanahabari na Wananchi,

Ugonjwa huu unapimwa kwenye vituo vyetu ambapo Serikali inaendelea kuimarisha upatikanaji wa vipimo vya ugonjwa huu na niwatake watoa huduma za afya wote na wananchi watambue kuwa **si kila homa ni dengue**, chunguza au chunguzwa maradhi mengine na wataalamu kwenye vituo vyetu vya huduma kwanza.

Mpaka sasa vituo vinavyopima ugonjwa wa homa ya Dengue ni pamoja na Muhimbili, Maabara kuu Muhimbili, Amana, Temeke, Mwananyamala, Sinza, Vijibweni, Mnazi mmoja, Lugalo, Mbagala, FFU Ukonga Katika Mkoa wa Dar es Salaam na vituo vya Bombo na Horohoro katika mkoa wa Tanga, Tumbi Mkuranga, Utete Rufiji na Mafia, Morogoro na Manyara Aidha natambua vipo pia vituo binafsi vinavyotoa huduma za upimaji. Katika mikoa mingine ufuatiliaji unaendelea na hatujapa wagonjwa wenye dalili za Homa ya Dengue.

Nipende kuwafahamisha pia kuwa Serikali imeagiza vipimo vingine vya kupima wagonjwa 30,000 ambavyo vinatarajia kuingia nchini hivi karibuni na vitasambazwa kwenye vituo vyetu vya umma katika mkoa wa Dar es Salaam na pia kwenye Mikoa mingine.

Ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja mpaka sasa na niwatahadharishe wanaoendelea kutoa taarifa za upotoshaji kuhusu tiba ya ugonjwa huu kupitia mitandao ya kijamii.

Ndugu Wanahabari na Wananchi.

Niwakunbushe tena wananchi **Kinga ni Bora kuliko Tiba** Jikinge na Ugonjwa huu wewe mwenyewe, kaya na familia yako pamoja, majirani pamoja na jamii yote.

Ndugu Wanahabari na Wananchi,

Wizara inaendelea kupongeza hatua zinazochukuliwa na mkoa wa Dar es Salaam katika kuudhibiti ugonjwa huu ambapo zoezi la kunyunyizia dawa viuadudu (Biolarvicides) kwa ajili ya kuangamiza mazalia ya mbu limekuwa likiendelea sambamba na kutoa elimu juu ya kujikinga n.k.

Pamoja na yote yanayofanyika niwaombe muongeze kasi, tumieni kamati za kitaalamu katika kudhibiti shirikisheni sekta zote pamoja na jamii na chukueni hatua kwa mujibu wa sheria kwa wote wanaovunja sheria za usafi wa mazingira na kusababisha mazalia ya mbu au kutochukua tahadhari.

Wizara inawakumbusha Viongozi wote katika Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Tarafa, Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji pamoja na maafisa wa afya nchini kuchukua hatua kwa dhati na wasidhanie kuwa ugonjwa huu uko ukanda wa pwani tu, bali unaweza ukatokea pia katika maeneo yao kwani mbu hawa wapo pia. Tunasisitiza kuwa ugonjwa huu unazuilika tushirikiane **kudhibiti mbu** kwani kwa kufanya hivyo pamoja na kudhibiti ugonjwa huu tutadhibiti pia magonjwa mengine yanayoenezwa na mbu.

Ndugu Wanahabari na Wananchi,

Niwatake tena Wananchi wote katika maeneo yao waongeze kasi ya kuangamiza mazalio yote ya mbu kwa kufanya yafuatayo;

1. Kufukia madimbwi ya maji yaliyotuama au kunyunyuzia dawa ya kuua viluwiluwi vya mbu kwenye madimbwi hayo
2. Kuondoa vitu vyote vinavyoweza kuweka mazalio ya mbu kama vile, vifuu vya nazi, makopo, magurudumu ya magari yaliyotupwa hovyo, nk.
3. Kufyeka vichaka vilivyo karibu na makazi ya watu
4. Kuhakikisha maua yanayopandwa kwenye makopo au ndoo hayaruhusu maji kutuama
5. Kufunika mashimo ya maji taka kwa mfuniko imara
6. Kusafisha gata za paa la nyumba ili kutoruhusu maji kutuama

Sambamba na hatua hizo, Wananchi wanaaswa kuendelea kuchukua hatua za kujikinga kuumwa na mbu ikiwa ni pamoja na;

1. Kutumia dawa za kufukuza mbu "mosquito repellants"
2. Kuvaa nguo ndefu kujikinga na kuumwa na mbu
3. Kutumia vyandarua vyenye viuatilifu (hata kwa wale wanaolala majira ya mchana)
4. Kuweka nyavu kwenye madirisha na milango ya nyumba za kuishi

Ndugu Wanahabari na Wananchi,

Wizara pamoja na Mikoa na Halmashauri tunachukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango wa dharura kukabiliana na ugonjwa huu, kuendeleza mapambano ya kudhibiti mbu, kuandaa mwongozo wa matibabu ya

ugonjwa huu, kuimarisha ufuatiliaji, kutoa elimu. Aidha Wizara pia imetuma timu za wataalamu kuungana na timu za mkoa wa Dar es Salaam ili kuudhibiti ugonjwa huu.

Hitimisho

Wizara inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa ugonjwa huu wa Homa ya Dengue nchini. Aidha, Wananchi wanashauriwa kujikinga na kuendelea na shughuli zao kama kawaida, kutokuwa na hofu na kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mara waonapo dalili za ugonjwa huu kama zilivyoainishwa hapo juu. Jamii inashauriwa kuhakikisha kuwa mazalio yote ya mbu yanaangamizwa hasa kipindi hiki cha mvua. Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wote wa sekta na mashirika mbalimbali kufuatilia na kudhibiti ugonjwa huu.

Imetolewa na

Prof. Muhammad Bakari Kambi

MGANGA MKUU WA SERIKALI